

# Mazoezi yaliyofanyika wakati wa warsha kuhusu 'Elimu-Jumuishi kwa Vitendo'

Zanzibar, 7-10 Februari 2006



**Imechapishwa na:**

The Atlas Alliance  
Schweigaardsgt 12  
SLP 9218 Grønland  
0134 Oslo, Norway  
Simu: +47 22 17 46 47  
Faksi: +47 23 16 35 95  
Barua pepe: atlas@atlas-alliansen.no  
Tovuti: www.atlas-alliansen.no

**Toleo la kwanza:** 12 machi 2007

**Mwandishi wa ripoti:** Ingrid Lewis

**Upatikanaji:**

Ripoti hii inapatikana kwenye tovuti ya 'Atlas Alliance':  
([www.atlas-alliansen.no](http://www.atlas-alliansen.no)), na vilevile unaweza kupata kwenye tovuti  
ya 'The Enabling Education Network': ([www.eenet.org.uk](http://www.eenet.org.uk)).

Vilevile ripoti hii inapatikana kwenye mfumo wa breili (Braille) na Kwa  
lugha ya Kiswahili kutoka shirika la 'Atlas Alliance'.

# Yaliyomo

<b>Yaliyomo.....</b>	<b>3</b>
<b>1. Utangulizi .....</b>	<b>4</b>
1.1. Ripoti hii .....	4
1.2. Njia zilizotumika wakati wa warsha .....	4
<b>2. Kipindi cha stadi za mawasiliano.....</b>	<b>6</b>
2.1. Kwa nini tulikiweka kipindi hiki? .....	6
2.2. Wasiwasi katika mawasiliano .....	6
2.3. Kuwawezesha wanasemina kuchanganyikana .....	7
2.4. Warsha sadifu .....	8
2.5. Mahojiano kwa njia ya masimulizi ya hadithi.....	11
2.6. Kurejea ujuzi na uzoefu binafsi .....	12
<b>3. Mazoezi makuu wakati wa warsha .....</b>	<b>16</b>
3.1. “Kubali-kataa” .....	16
3.2. Kutafsiri elimu-jumuishi .....	16
3.3. Je elimu-jumuishi inaonekanaje? .....	16
3.4. Elimu-jumuishi ni mchakato endelevu unaowahakikishia wanafunzi kuwepo, kushiriki na kunufaika (kupata maarifa).....	17
3.5. Vikwazo na utatuzi/ufumbuzi.....	17
3.5.1. Uchunguzi wa picha .....	17
3.5.2. Vielelezo vya mlima.....	18
3.5.3. Uzoefu binafsi na kuandika .....	19
3.5.4. Maigizo/michezo ya kuigiza.....	20
3.5.5. Kutembelea/ziara mashuleni .....	20
<b>4. Mazoezi ya chemsha-bongo .....</b>	<b>23</b>
4.1. Michezo ya furaha ya kuvunja ukimya .....	23
4.2. Michezo kuvunja ukimya inayohusisha elimu-jumuishi .....	24
<b>Viambatisho .....</b>	<b>25</b>
Kiambatisho cha 1: Matumaini na mashaka ya washiriki kuhusu warsha .....	25
Kiambatisho cha 2: Mtandao bayana (swap-shop networking) .....	27
Kiambatisho cha 3: Mapendekezo ya marejeo ya kusoma .....	32

# 1. Utangulizi

## 1.1. Ripoti hii

Ripoti hii inatoa habari mbadala kutoka kwenye ripoti kuu ya warsha ya “Elimu-jumuishi kwa Vitendo: Ripoti ya warsha ya elimu jumuishi ya tarehe 7-10 Februari 2006”.<sup>1</sup> Ripoti kuu ina maelezo ya kina kuhusu majadiliano na matokeo kutoka warsha ya Atlas alliance. Katika ripoti hii inaelezea baadhi ya mazoezi muhimu yaliyotumika wakati wa warsha na kutoa maoni juu ya umuhimu wake. Ripoti hii ni muhimu ikasomwa sambamba na ripoti kuu.

## 1.2. Njia zilizotumika wakati wa warsha

Warsha ilitarajia washiriki wajifunze kutokana na uzoefu wa kila mmoja wao; ikiwa ni pamoja na mawazo, mipango, utekelezaji na mapitio ya kazi za elimu-jumuishi katika mazingira ya nchi inayoendelea. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha washiriki kufikiri kuhusu mipango yao ya baadae juu ya elimu-jumuishi. Katika mchakato mzima wa kutoa habari kuhusu elimu-jumuishi, warsha vilevile ilionesha njia shirikishi ambazo wanasemina wangeweza kuzitumia katika kazi yao na kuonyesha ufafanuzi baadhi ya njia za kufundishia na kujifunza ambazo mara kwa mara hubainisha darasa-jumuishi .

### Njia shirikishi katika kujifunza

Njia shirikishi katika kujifunza ilipewa kipaumbele katika muda wote wa warsha. Njia hii ilihamasisha wanasemina kushiriki zaidi katika mazoezi - na kwa kiwango fulani iliwasaidia pia kushiriki katika kujifunza . Njia hii ilileta msukumo katika kutafuta majibu na kuunganisha taarifa pamoja kutoka nyanzo mbalimbali; badala ya kumtegemea tu mwalimu au mkufunzi kuongoza vipindi vyote vya masomo. Kwa sababu elimu-jumuishi si dhana rahisi ambayo inaweza kutumika kwa namna moja katika sehemu zote, wanasemina katika warsha za elimu-jumuishi wanapaswa kupewa mwongozo wa kutafuta na kupata habari sahihi na kutafuta njia bora ya kusonga mbele kwa kuanzia sehemu walizopo.

Zaidi ya mazoezi yaliyokuwa yamepangwa kwenye ratiba, ushirikishwaji katika kujifunza ulifanywa pia katika majadiliano ya nje wakati wa mapumziko, na katika maktaba ndogo ambamo washiriki waliweza kupata nafasi ya kujisomea kwa ziada.

### Njia mbalimbali za kujifunza

Warsha ilitumia kazi za vikundi na jozi, majadiliano ya wazi, uwasilishaji wa mada, na maigizo. Njia zote hizi zilisaidia wanasemina kuona/kutafuta ni njia ipi inamfaa, kwa kuwa si kila mmoja anapendelea kujifunza kwa kutumia njia sawa na ya mwenzake.

---

<sup>1</sup> Atlas Alliance (2007) “Ujumuisho katika Vitendo: Ripoti ya warsha kuhusu elimu-jumuishi, Zanzibar, 7–10 Februari 2006” / inapatikana kutoka Atlas Alliance kwenye tovuti ([www.atlas-alliance.no](http://www.atlas-alliance.no)) au kutoka kwenye tovuti ya shirika la The Enabling Education Network ([www.eenet.org.uk](http://www.eenet.org.uk)).

Mazoezi mbalimbali pia yalitumika ili kusadifu njia zilizotumika, na kuweza kufafanua kwa uhakika ni jinsi gani kujifunza kwa darasa jumuishi kunavyoweza kufanya kazi.

Uzoefu wote ni muhimu

Warsha ililenga kuendeleza dhana kwamba hupaswi kujifanya mjuaji zaidi wa elimu-jumuishi kwa kufanya peke yako matendo ambayo unadhani yanaifanya elimu iwe jumuishi zaidi. Kila mmoja ana mawazo na uzoefu wake ambapo vyote ni muhimu katika kuendeleza mfumo wa elimu-jumuishi na jamii nzima. Kwa hiyo warsha ilitumia ‘mazoezi mengi’<sup>2</sup> kuonyesha umuhimu wa kujifunza kutokana na mawazo na uzoefu wa mtu mmoja mmoja pamoja na kujifunza mawazo na uzoefu wa wataalam wa elimu-jumuishi.

---

<sup>2</sup> Kwa mfano, mahojiano ya masimulizi ya hadithi (taz: kipengere 2.6) na mazoezi ya ‘kutangaza ujumuishi’ (taz: kipengere 2.7) vipengere vyote viwili vimeonyesha uzoefu binafsi wa washiriki, na si lazima iwe katika kazi ya elimu jumuishi.

## 2. Kipindi cha stadi za mawasiliano

### 2.1. Kwa nini tulikiweka kipindi hiki?

Ingawa tunatumia uwasilishaji wa mada au kutumia kazi za vikundi, tunahitaji aina stadi maalum za mawasiliano. Tunapaswa kuwaelezea watu kuwa kuhusu sisi wenyewe, kazi zetu, uzoefu wetu au mawazo yetu, na mara kwa mara tunahitaji uwezo wa kufanya hivi kwa muda mfupi. Ni kawaida kwa wanasemina kukosa ujuzi na/au kutojiamini katika mawasiliano. Hii inaweza kuathiri maendeleo na matokeo ya warsha hasa ukizingatia kwamba mwanasemina wanatarajiwa kuchangia hoja na uzoefu, na sio kuwa msikilizaji tu.

Kwa hiyo siku ya kwanza ya warsha ya 'Elimu-jumuishi kwa Vitendo' ilianza kwa kuwasaidia wanasemina kujiamini kama wazungumzaji na wasikilizaji. Wakati huu wanasemina waliweza kuelezea uzoefu wao binafsi kwa kuonyesha ya kwamba hawakuanza warsha bila ya kuwa na ujuzi wowote. Mbinu za mawasiliano na mambo yanayofanikisha warsha kwa jumla, pia yalizingatiwa.

Kwa kutumia muda wa awali kwa maandalizi ya wanasemina ni kigezo kizuri kama njia ya kuongeza ushiriki wao na kufaidika kwao katika tukio zima la warsha.

### 2.2. Wasiwasi katika mawasiliano

Kuwahamasisha wanasemina kufikiria nini wanachotakiwa kupata kwenye warsha na nini wasiwasi wao juu ya warsha. Hii inaweza kusaidia kuelewa mahitaji na matakwa ya wanasemina na masuala ya mawasiliano. Kabla ya warsha, maswali ya dodoso yalitolewa na kujazwa na wanasemina. Katika sehemu moja ya dodoso walitakiwa kutaja mambo ambayo wangependa kujifunza na kuvipitia wakati wa warsha<sup>3</sup>. Yafuatayo ni mambo yanayohusiana na mawasiliano kama yalivyofafanuliwa na washiriki wakisaidiana na mwendeshaji wa warsha.

---

<sup>3</sup> Tazama kiambatisho cha 1 kuhusu majibu mbalimbali ya wanasemina.

<b>Maoni ya washiriki</b>	<b>Majibu ya mwendeshaji</b>
Matumizi ya muda – wasiwasi wa kutokuwa na muda wa kutosha wa majadiliano/uwasilishaji.	Wote tunaweza kuokoa muda kwa kuwahi asubuhi na baada ya mapumziko! Tufanya vitendo ambavyo vitasaidia kufanya mazoezi ya namna ya kusimulia hadithi na kuwasiliana.
Kukosekana kwa uzoefu – wasiwasi wa kutokuwa na cha kuzungumza.	Kila mmoja anao uzoefu unaohusiana na warsha hii, hata kama haukupatikana moja kwa moja katika elimu-jumuishi. Bado mtakuwa na mengi mazuri ya kuchangia.
Washiriki wamegawanyika mno – kiasi kwamba itakuwa vigumu kwa wanasemina kujadiliana kutokana na historia tofauti na kiwango tofauti cha uzoefu na nchi walikotoka.	Mgawanyiko ni hazina ya maendeleo, ukweli ni kwamba watu kutoka historia tofauti wanaleta maana ya kujifunza elimu-jumuishi na jamii-jumuishi kwa mtazamo na mawanda mapana zaidi.
Baadhi ya watu huenda wasiwe tayari kubadilishana ujuzi/mawazo yao na wengine – ni namna gani tutawafanya wazungumze.	Wote tupo hapa ili kubadilishana mawazo na uzoefu, na washiriki wote ni sawa; hivyo hakuna haja ya mashaka, au hali ya kutotaka kubadilishana ujuzi na mawazo. Tutatumia njia mbalimbali ili kumuwezesha kila mmoja kuwa na furaha katika kuongea na kubadilishana mawazo na ujuzi.
Huenda kukawa na mabishano au kutokuelewana kuhusu kilichozungumza au kuwasilishwa.	Warsha hii sio ya kutoleana hukumu dhidi ya hoja au mawazo ya mwingine kuhusu elimu-jumuishi; hakuna atakayekubaliwa kupinga au kukosoa kazi za wengine bila kuchangia mawazo endelevu na yenye kujenga na kusaidia na kuboresha kazi.

### **2.3. Kuwawezesha wanasemina kuchanganyikana**

Katika warsha tunapenda kukaa na watu tunaowajua – haipendezi kuchanganya kundi kubwa la watu usiowajua wala kukutana nao kabla. Hata hivyo kama wanasemina hawatachanganywa basi warsha inakuwa dhahifu na isiyoleta changamoto katika kubadilishana mawazo na uzoefu. Mtandao wa 'swap shop' ni mchezo wa kuvunja ukimya ambao pia unaweza kutumika kuleta changamoto katika mjadala wa mada husika.

Wanasemina walipewa vikaratasi (vyenye gundi) na waliulizwa kuandika majibu ya maswali haya mawili katika karatasi za kubandika na majina yao;

- “Kuhusiana na elimu-jumuishi, ninataka kujua...”
- “Kuhusiana na elimu-jumuishi naweza nikachangia.....”

Wanasemina kisha walibandika karatasi zao katika mabango yaliyoandikwa “Nataka kujua...” na “Naweza nikachangia...”<sup>4</sup> Walihamasishwa kila mmoja kutafuta mtu ambaye wanamechi. Kwa mfano, kama mtu mmoja alitaka kujua jinsi ya kufanya kazi na makundi ya wazazi, basi alitakiwa kuangalia mshiriki mwingine ambaye anaweza kuelezea uzoefu wa kufanya kazi na wazazi; kisha kukaa pamoja na kubadilishana mawazo kuhusu mada.

Baada ya aibu kidogo, washiriki walianza kutafuta watu wanaolingana kwa mahitaji yao na majadiliano ya moja kwa moja yakafuata. Makundi madogomadogo ya washiriki yalitengenezwa yenye mahitaji sawa na kuanza kujiunga na vikundi vya wawili wawili wenye kutegemeana. Kwa kuwa hii ilikuwa ni kama mchezo wa kuvunja ukimya ilitumia kama dakika 15 ambazo hazikutosha kwa washiriki kumaliza mazungumzo yao. Hata hivyo mwendesha-warsha aliwaambia washiriki kuendelea na majadiliano kwa wiki yote wakati wa vipindi vyote vya mapumziko. Tathmini ya mwisho wa warsha iliashiria kuwa washiriki wengi



*Mtandao (mchezo) wa 'swap-shop'*

## 2.4. Warsha sadifu

Kusadifu kwa warsha ni zaidi ya mawasiliano ya kuona na kusikia au kuyazoea mazingira ya sehemu ya warsha. Mazingira yaliyotengenezwa wakati wa warsha yana mchango mkubwa kwa kuwajumuisha washiriki na kupata maarifa waliyotarajia. Tilitumia baadhi ya muda kuangalia masuala yanayoifanya warsha isadifu ili tujiwekee misingi itakayotuongoza kwa kipindi chote cha warsha.

### ***Uchambuzi wa picha***

Wanasemina walioneshwa picha mbili za warsha. Picha zilioneshwa kwenye skrini (*overhead screen*) na nakala za picha hizo ziliprintiwa na kusambazwa. Washiriki walifanya kazi kwa makundi ya watu 4 mpaka 5. Washiriki walitakiwa kujadili maswali yafuatayo:

- Unafikiria nini kinatokea katika kila picha?
- Elezea mazingira katika kila picha?
- Ni jinsi gani watu wanahusiana?

<sup>4</sup> Tazama kiambatisho cha 2 kuhusu na majibu ya washirikiki.



- Unazionaje picha hizi ukilinganisha na uzoefu wako wa vikao na warsha.

Kulikuwa na majadiliano hai yenye vicheko katika makundi yote. Picha zilichangamsha majadiliano katika mada zote kama vile “jinsi gani mtu mmoja anaweza kutumia njia ya kazi za vikundi katika darasa lenye wanafunzi 80?”. Washiriki pia walitoa mapendekezo mbalimbali kuhusu tabia na hisia za watu katika picha.



*Picha (a)*

Washiriki walisema kuwa watu wengine katika hali hii walionekana kuchoka, kulala, kugilibiwa; hawamsikilizi mwasilishaji - inaonekana kama walikuwa wakicheka na kutaniana, nk.



*Picha (b)*

Washiriki walipendekeza kuwa picha hii inaonesha zaidi ushiriki hai, majadiliano hai, kuipenda mada, kila mmoja anaonekana kushiriki.

Kumbuka: Picha hizi mbili zilipigwa tu saa moja wakati wa warsha hiyo. Picha ya kwanza inaonyesha kipindi cha ufunguzi, wakati huo viti vilipagwa kulingana na uzoefu wa washiriki katika warsha zilizopita. Na picha ya pili inaonesha waendeshaji walibadilisha mpangilio wa ukaaji ili kuwezesha ushirikishaji zaidi kuchukua nafasi yake.

Baada ya kupata changamoto ya picha washiriki waliulizwa kutoa mapendekezo kuhusu mambo yanayoweza kuifanya warsha kusadifu. Walipata mawazo kutokana

na picha hizo na uzoefu walionao katika warsha na vikao. Hivyo walihitimisha yafuatayo:

### ***Vitu gani vinaifanya warsha isadifu/nzuri?***

- kukubali na kuheshimu.
- kusikika
- kuendana na mahitaji maalumu kwa mfano lugha ya ishara. Pia wakati wa kufanya kazi na washiriki walemavu wasioona, watu wawili wawaelezee picha kwao.
- usidharau au kupinga mawazo
- kila mmoja ashirikishwe katika mjadala (vikundi vidogo vitumike kwa hili)
- kutumia muda ipasavyo (ingawa pia inatakiwa kubadilika na kutozuia mjadala wa somo kwa sababu ya ratiba iliyopangwa.)
- kama mtu asiposhiriki nasi, tunaweza kumhamasisha
- ujumuishi
- kukubali kubadilishana mawazo
- lugha na uelewa (washiriki wanatakiwa kusema kama hawaelewi)
- kufurahi
- kujifunza kufanya kazi katika vikundi.
- kuhusisha mada na washiriki
- haja ya kuwachanganya washiriki (wa nchi mbalimbali, jinsia, kwa aina ya kazi, n.k.)
- malengo kueleweka kwa kila mtu (washiriki wanapaswa kumkumbusha mwendeshaji kuelezea malengo kama hayajaeleweka)
- kuwahamasisha washiriki kwa kuwapa mazoezi
- mwendeshaji
- mawasiliano ya pande zote mbili.
- uwezo wa kuona.

Mwendeshaji kwa kutumia projekta ya 'overhead' pia aliwasilisha baadhi ya mambo muhimu ya uendeshaji.

- usiongee haraka
- ielekee hadhira yako
- tumia maneno rahisi
- usitumie msamiati mgumu na vifupisho vya maneno
- andika maandishi makubwa na yakuonekana katika karatasi za manila na 'overhead' kwa kutumia rangi nzito
- soma na kuelezea kilichooneshwa kwenye 'overhead'
- usibananishe mambo mengi katika ukurasa mmoja.
- chukua mapumziko ya kawaida
- mwambie mwenzio kama hujaelewa, kuona, kusikia au haufurahii.

Ilisisitizwa kuwa ni majukumu ya kila mshiriki sio tu majukumu ya mwendeshaji na mwandaaji – kuhakikisha kuwa vipengele vyote hivi na "warsha nzuri" vinafuatwa. Wakati wa warsha washiriki wengi waliwaomba waendeshaji kwenda taratibu, kuelezea tena, au kusogezwa ili kuonekana vizuri kwenye skrini (overhead).

### ***Masomo yajumuishayo washiriki wasioona katika shunguli za uchambuzi wa picha***

- Matumizi ya picha na taswira zingine hayahusishi mazoezi ya wanasemina wanaoona tu.
- Hakikisha kuwa angalau watu wawili katika kikundi wanawaelezea picha washiriki wasioona (kwa kuwa kila mmoja ataona na kuzingatia mambo mbalimbali katika picha.)
- Mwendeshaji anaweza kuwasaidia washiriki katika kikundi ambao hawawezi kuelezea.
- Kwa kusikiliza ufafanuzi wa picha inaweza kumsaidia mshiriki asiyeona kufuatilia kwa kina mada zinazojadiliwa, na hata wanaoona vizuri pia watanufaika kwa kuona picha kwa karibu na kuzichambua, wanaweza pia kuona vitu ambavyo hawakuwa wameviona vizuri.
- Uchambuzi wa picha ukiwasilishwa vizuri inaweza kuwa njia nzuri ya kuwashirikisha washiriki wasioona katika majadiliano ya vikundi.

## **2.5. Mahojiano kwa njia ya masimulizi ya hadithi**

Katika warsha tunapaswa kutoa taarifa kuhusu uzoefu au mawazo katika muda mfupi, na pia tunapaswa kusikiliza taarifa zinazotolewa na waendeshaji wengine. Wakati mwingine tunakosa au hatuelewi vizuri kama hatukusikiliza kwa umakini. Zoezi la masimulizi ya hadithi liliwapa washiriki nafasi ya kufanya mazoezi ya kutoa taarifa sahihi na muhimu kuhusu uzoefu kwa muda wa dakika tano, na kufanya mazoezi ya kusikiliza kwa makini ili waweze kuisimulia hadithi tena. Kazi hii pia imeundwa kuwasaidia washiriki kuanza kutafakari juu ya uzoefu wao binafsi kuhusu masuala ya ujumuishi na usawa.

Washiriki walitakiwa kukaa katika vikundi vya wawili wawili (na mtu ambae hawamjui) Walitakiwa kufikiria kuhusu kitu walichokifanya kuhamasisha ujumuishi au haki sawa kwa mtu au makundi ya watu ambao wanatengwa (sio lazima katika elimu).Walipewa dakika tano za kuwasimuliana hadithi. Mshiriki-mwenza alikuwa msikilizaji, aliandika yale muhimu kwa kifupi kuhusu hadithi. Mtu hakuruhusiwa kumkatiza msimuliaji. Baada ya hadithi kumalizika, msikilizaji alitumia nukuu zake kuisimulia upya hadithi kwa mwenzake aliyeisimulia kwanza. Na kisha walijadili hadithi na kupeana majukumu.

Majadiliano ya wazi (wote) kuhusu zoezi hilo yalifanyika.Washiriki waliulizwa kutoa maoni yao jinsi gani walivyojisikia au kama kulikuwa na tatizo lolote au chochote muhimu katika zoezi hilo.

### ***Vikwazo***

- Ilikuwa ngumu kuandaa hadithi kwa muda mfupi; wakati mwingine nafikiria kujazia vitu nilivyosahau.
- Kujaribu kuifanyia kazi hadithi kwa muda mfupi ilikuwa ngumu kwangu; kwa sababu ilibidi kutafsiri kwa kutumia lugha yangu.
- Muda hautoshi wa kumuuliza maswali msimuliaji hadithi.
- Kwa muda huu mfupi unapelekea kuelezea vitu ambavyo ni rahisi kuelewa kuliko kitu muhimu.

- Ni vigumu kusikiliza kwa dakika tano bila kuuliza swali, ni adhabu kwa njia nyingine!
- Inanipa hamu ya kusikiliza hadithi nzima

### *Muhimu*

- Kusikiliza kunamhamasisha mwenzako
- simulizi hizi za hadithi zimetuweka karibu
- Nzuri “kubadilisha mazingira”
- Muhimu kuandika mambo muhimu ili kukumbuka.
- Usikilizaji wa makini unakufanya kuuliza maswali machache, kwa hiyo sio ukimya moja kwa moja.
- Ni vizuri kuwa makini wakati wote
- Tuliibu uzoefu ambao tunahitaji kubadilishana.
- Nilijaribu kuunda picha katika akili yangu, kuhusisha kile mwenzangu alichokuwa akinihadithia.

Washiriki walikumbushwa kuwa mbinu hizi za kuongea na kusikiliza ni mbinu ambazo walitakiwa kuzitumia wakati wote wa warsha. Pia ni mbinu muhimu za kutumia katika kazi zao za kila siku.

Baadhi ya changamoto ambazo washiriki walipata kuhusu hadithi simulizi zinatatulika kwa kufanyia mazoezi. Kama tukirejea uzoefu wetu kazini tutapata kueleza umuhimu – badala ya urahisi wa kusimulia hadithi kwa muda mfupi.

Zoezi hili lilisaidia kuwakumbusha washiriki kuwa hadithi simulizi zenye uzoefu wa mtu binafsi ni sehemu muhimu ya kubadilishana mawazo, ambayo ni shughuli muhimu katika maendeleo ya elimu-jumuishi. Kila mara tunaposimuliana hadithi tunafikiria habari mpya muhimu, au tutatafuta njia mpya ya kuchambua taarifa ambayo itatusaidia katika mchakato wa kutatua matatizo.

## **2.6. Kurejea ujuzi na uzoefu binafsi**

### *Lengo*

Mara nyingi warsha za ushirikishaji huweza kuhofiwa. Washiriki wanaweza kuogopa kuwa hawajui vya kutosha kuhusu somo fulani na kwa hiyo watagombania kujiunga. Warsha pia mara nyingine huhufanya masomo magumu – vikwazo ambavyo tunajaribu kuvishughulikia. Kwa hivyo zoezi lifuatalo lililenga kuwasaidia washiriki kuanza warsha wakiwa na imani nzuri kuhusu mambo waliyokuwa na uzoefu nayo kabla. Iliwasaidia kujiamini na ujuzi ambao tayari walikuwa nao kuweza kufanya kazi za elimu-jumuishi na masuala ya usawa.

### *Mchakato*

Washiriki walipangwa kufuatana na kazi wanazofanya. Hata hivyo waliruhusiwa kuchagua makundi yao, badala ya kuambiwa kundi gani watajiunga nalo. Baadhi ya washiriki walichagua kujiunga makundi ambayo mwendeshaji hakutegemea kabisa kuonyesha kuwa mtazamo wa kazi zetu unaweza kuwa tofauti na jinsi wengine wanavyoona.

Vikundi vilikuwa kama ifuatavyo:

- walimu na walimu wakuu
- wafanyakazi wazalendo katika mashirika ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikari NGOs
- wafanyakazi wa kimataifa wanaofanya kazi katika mashirika yasio ya kiserikari kutoka makao makuu
- maafisa elimu na wakaguzi (walikuwa wengi kwa hiyo walikaa katika vikundi viwili)
- wazazi, mashirika ya wazazi, mashirika ya walemavu.

Washiriki walipewa maelekezo yafuatayo:

- **Jifanye** kuwa mdhamini anatoa fedha kudhamini miradi, mashule, wizara, n.k. ambayo itaonesha kuwa wanafanyakazi katika elimu-jumuishi au katika shughuli nyingine za kufanya jamii kuwa sawa na jumuishi kwa kila mtu.
- Mdhamini anawataka waombaji kuandika matangazo ambayo yanaonyesha mambo yote waliyofanya kuwezesha shule na jamii kwa ujumla kuwa jumuishi zaidi. Matangazo pia yanaweza kuonesha *ujuzi na mwelekeo* mzuri wa wafanyakazi katika huo mradi/shule/wizara.
- Linatakiwa lionekane kama tangazo (mfano kama ya kwenye magazeti au mabango barabarani) fupi, la kuvutia, na zuri.
- Kabla ya kutengeneza bango la tangazo, jadilianeni kimakundi kutafuta ujuzi, mwelekeo, na uzoefu, ambao utatajwa kwenye bango.
- Unatakiwa kuwa mkweli asilimia 100.
- Utaona ni muhimu kuanza na sentensi hii : “Sisi ni mradi/shule/wizara muafaka tunaostahili kupewa mchango wa fedha kwa ajili ya kuboresha na kudumisha elimu-jumuishi/jamii-jumuishi kwa sababu.....”

Washiriki walilionga zoezi hili kuwa gumu; na hii inawezekana ni kutokana na sababu zifuatazo:

- *Hatujazoea kuongelea kuhusu imani zetu binafsi na uzoefu kuhusiana na kazi.* Kazi yetu mara nyingi hatuithamini na wakati mwingine tunashusha thamani ya ujuzi wa mtu alionao. Ukweli ni kuwa bado watu ndio wanaoweza kuiwezesha jamii iwe au isiwe jumuishi. Kwa hiyo sisi sote tunahitaji kujipanga upya na matendo na imani zetu, bila kuhofia kupoteza hadhi za profesheni zetu.
- *Hatujazoea kufikiria na kuwasilisha mawazo yetu kwa njia mbaimbali.* Tumezoea kuandaa/kuandika maombi kiofisi kwa kufuata kanuni zinazotambulika, ili kuwavutia wahisani. Mara nyingi tunapata elimu inayotulazimisha kufuata kanuni tu badala ya kuwa wabunifu; kwa hiyo kubuni na kuandaa tangazo la kuchekesha lenye kubeba ujumbe kwa lengo la kuufikisha ujumbe huo kwa jamii ni kitu ambacho hatujakizoea. Lakini bado inawezekana kuwa kama njia moja ya kufikisha taarifa. Kwa hiyo tunatakiwa kufanya mazoezi kwa kutumia hii mbinu ya ubunifu wa mawasiliano, hasa tunavyofanya kazi na watoto. Labda pia haikufafanuliwa kwa uwazi zaidi na waendeshaji kuwa huu ulikuwa ni *mfano halisi*, ndio maana wengine hawakulielewa vizuri zoezi hili na hivyo kufikiri kuwa linawafundisha mbinu mpya za kuandika maombi ya mradi.

Katika warsha hii, ukosefu wa muda umezuia vikundi kuwasilisha kazi zao za kivitundi katika majadiliano ya wazi.

Badala yake mtu mmoja kutoka katika kila kikundi alisimama mbele ya bango lao kuelezea zaidi; na wakati wengine walikuwa wanazunguka kuangalia bango lao na kujadiliana yaliyomo. Majadiliano marefu ya pamoja yangeweza kusaidia kufuta vitu ambavyo havieleweki kuhusu zoezi zima.

Licha ya vikwazo katika zoezi hili, lilitoa changamoto ya majadiliano na vipeperushi vyenye maelezo ya kina. Zoezi pia lilisaidia kuonesha baadhi ya uwezo wa mbinu, tabia na uzoefu ambao unatusaidia katika kusonga mbele katika kazi jumuishi ambayo kwamba wengi wa washiriki tayari walikuwa nayo (tazama orodha hapo chini). Washiriki walielezwa kuangalia vipeperushi na kujikumbusha ujuzi na uzoefu walio nao kama watakuwa hawana uhakika wa uwezo wao katika warsha.

- stadi wa kuhasusha wazazi
- kujifunza kutokana na uzoefu binafsi
- maarifa ya elimu-jumuishi
- maarifa juu ya mahitaji na haki za watoto
- uzoefu mkubwa katika kushawishi kuwepo kwa sera za elimu-jumuishi.
- kufanya kazi na wataalamu wa afya, elimu, CBR
- uwezo wa kuwasiliana na mashirika ya wasiojiweza na mamlaka ya serikakari za nchi husika.
- “kwa pamoja tunaweza”.
- tunaamini kuwa tukijituma, hata kidogo tulichonacho tunaweza kuisaidia jamii yetu.
- sisi tuna:
  - ♦ mtandao wa rasilmali (nguvu kazi na vifaa)
  - ♦ uzoefu kutokana na mahusiano na vikundi vya kimataifa na serikali
  - ♦ maarifa ya kina kwenye kazi za jamii; mahitaji maalum; mazoezi-jumuishi; utaalamu wa tamaduni mbalimbali; umilisi wa lugha
- ni walimu wazoefu. Tunajua namna ya:
  - ♦ kuwaleta wazazi pamoja na kujadiliana kuhusu umuhimu wa shule
  - ♦ kuwaandaa watoto kuwa na uwezo wa kutenda wenyewe
  - ♦ kuandaa warsha/semina kwa wazazi na walimu
  - ♦ kutumia vifaa vya kienyeji kutathmini, kufundishia na kujifunza.
  - ♦ kuwasikiliza watoto na wazazi.
  - ♦ kuifikia jamii kwa kutumia televisheni na vipindi vya radio
  - ♦ kutengeneza hali ya kuwa tayari kubadilika
  - ♦ kutambua watoto walemavu shuleni na kuwawezesha wajifunze.

## 2.7. Kurejea mazoezi ya stadi za mawasiliano

Wanasemina walitakiwa kutoa maoni kwa namna gani mazoezi ya stadi za mawasiliano hapo juu yanaweza kuendana na zoezi zima la elimu-jumuishi. Walitoa mawazo yafuatayo:

- Naweza kuyatumia yote kwenye mafunzo ya walimu na wanafunzi.
- Katika mazingira yetu ya shule tunaweza kuzitumia kidogo tu baadhi ya hizo mbinu. Walimu wanaweza kuwa katika vikundi vidogovidogo kutengeneza zana [za kufundishia/kujifunza].
- Utendaji umekuwa jumuishi kutokana na utofauti wa wanakikundi (kitaifa/kiuwezo/kiuzoefu).
- Utendaji umekuwa shirikishi, na mazoezi/mbinu hizo zinaweza kutumiwa na wadau wote katika michakato tofauti na viwango vyote wakati wa kuanzisha elimu-jumuishi.



## 3. Mazoezi makuu wakati wa warsha

### 3.1. “Kubali-kataa”

Hili ni zoezi la chemsha-bongo ambalo pia hutoa changamoto kwa wanasemina kushiriki katika mdahalo wa maswali na majibu kuhusiana na mada watakazochagua katika warsha. Wanasemina walisimama upande mmoja wa chumba. Upande mwingine wa chumba alama mbili zilikuwa zimebandikwa ukutani moja ilisema “Kubali” nyingine ilisema “Kataa”. Mwendeshaji alisoma maelezo na wanasemina walitakiwa kuchagua upande wenye ama *kubali* au *kataa* kutegemeana na maoni au mawazo yao binafsi. Kama mwanasemina alishindwa au kukosa uamuzi wa sehemu gani achague, basi alitakiwa kusimama katikati. Wanasemina waliambiwa wawashawishi wenzao kuchagua au kubadili mwelekeo.

Maelezo yaliyosomwa katika zoezi hili yalitakiwa kuwa na kiwango cha kutolingana. Kwa mfano huu maelezo kutoka pande mbili yalishinda kuleta mvuto kwa wanasemina waliokuwa wanapingana kimtizamo. Lakini maelezo kuhusiana na endapo wasichana wakipata mimba waweza kuendelea na masomo yalizua kitimoto na mjadala mrefu. Hii ilikuwa njia ya kuwafanya wanasemina washiriki zaidi majadiliano katika warsha na wakati huo kuleta changamoto kwao kuhusiana na mada ambayo hapo kabla hawakuipa nafasi katika mjadala wa elimu-jumuishi.<sup>5</sup>

### 3.2. Kutafsiri elimu-jumuishi

Kipindi hiki kilihusisha chemsha-bongo ya pamoja kwa wanasemina kutoa maana ya ‘elimu-jumuishi’. Kulikuwa na tafsiri iliyotolewa na ‘EENET’ kuhusu ‘elimu-jumuishi’ ambapo washiriki pia walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu fasili hiyo. Vielelezo/michoro mbalimbali ilioneshwa kufafanua njia mbalimbali za kutatua tatizo la kushughulikia wanafunzi waliotengwa – kwa kumwangukia mtoto kama tatizo, na kisha kuuangalia mfumo wa elimu kama tatizo. Yote haya yalijadiliwa na kuibua tashwishi ya majadiliano kuhusu tafsiri hizo za ‘elimu-jumuishi’ na kuleta changamoto ya kutafakari jinsi ya kuitekeleza ‘elimu-jumuishi’ kwa vitendo.<sup>6</sup> Kutumia mchanganyiko wa chemsha-bongo, uwasilishaji na majadiliano, ilikuwa ni njia nzuri ya kuwahamasisha wanasemina kurejea na kufikiria tafsiri zao na welewa wao kuhusu dhana ya ‘elimu-jumuishi’, badala ya kuafikiana na maelezo yote wanayopewa na wakufunzi.

### 3.3. Je elimu-jumuishi inaonekanaje?

Zoezi hili nalo lilihusisha uchambuzi wa picha, kwa kutumia picha zilizopigwa na watoto wa shule nchini zambia na indonesia. Wanasemina walifanya kazi katika

---

<sup>5</sup> Maelezo ya mjadala huo yapo katika ripoti kuu: “Elimu-jumuishi kwa Vitendo: Taarifa ya warsha kuhusu elimu-jumuishi, 7 – 10 Februari 2006”.

<sup>6</sup> Maelezo ya chemsha-bongo, vielelezo na majadiliano yanapatikana katika ripoti ya “Elimu-jumuishi kwa Vitendo”.



vikundi walivyojichagulia wenyewe, na walipewa picha kadhaa kuziangalia. Waliambiwa kujadili maswali yafuatayo:<sup>7</sup>

- Picha gani unafikiri inaonyesha shule jumuishi au shule ambayo inaonyesha maendeleo ya kuwa jumuishi? Kwa nini?
- Ni jinsi gani unafananisha picha inayofanana na shule jumuishi kulinganisha na taswira unayofikiria kwa akili yako?

Muda wa ziada ulitolewa ili kuzisoma, kuzitafakari na kuzijadili picha hizo, na majadilino ya pamoja kwa ufupi pia yalifanyika. Zoezi hili pia lilisaidia kuelezea kwa ufasaha washiriki kuwa elimu-jumuishi ina sura nyingi – Kuna changamoto nyingi kuibadilisha elimu kuwa jumuishi zaidi; na wadau mbalimbali wanaweza kupata changamoto anuwai hata kama ni katika mazingira, sehemu, au eneo moja. Hatuwezi kutumia picha moja tu kuhakikisha kuwa shule ni jumuishi au la.

### **3.4. Elimu-jumuishi ni mchakato endelevu unaowahakikishia wanafunzi kuwepo, kushiriki na kunufaika (kupata maarifa)**

Sehemu hii ya warsha imeelezwa kwa njia ya uwasilishaji wa mada na majadiliano ya pamoja. Maelezo yake yametolewa katika ripoti kuu: “Elimu-jumuishi kwa Vitendo: Taarifa ya warsha kuhusu elimu-jumuishi, 7 – 10 Februari 2006”.

### **3.5. Vikwazo na utatuzi/ufumbuzi**

Kwa nyongeza kwenye utoaji mada kutoka kwa waendeshaji,<sup>8</sup> mazoezi makuu matano yalitumika wakati wa warsha kuwasaidia washiriki kukumbuka na kujadili masuala ya vikwazo na tatuzi katika elimu-jumuishi. Mazoezi hayo yalijumuisha: uchambuzi wa picha, vielelezo vya mlima, uzoefu-binafsi na kuandika, kufanya ziara mashuleni, na maigizo.

#### **3.5.1. Uchunguzi wa picha**

Washiriki wakiwa katika vikundi vidogo vidogo vilivyochaguliwa bila ya utaratibu maalum, yalipewa seti sita za picha kila kikundi. Kila kikundi kilikuwa na picha tofauti. Waliambiwa kuzichunguza na kutafuta vikwazo vingi iwezekanavyo kuhusu elimu-jumuishi. Walishauriwa kuangalia vikwazo vya wazi na visivyoonekana kwa uwazi, na pkisha kutafuta aina zote za vikwazo (vya kimazingira, tabia, sera, utendaji, na rasilimali).

Katika majadiliano ya pamoja washiriki waliorodhesha vikwazo mbalimbali walivyofikiria vilikuwepo kwenye picha. Walihamasishwa kufikiria kuhusu aina za vikwazo vilivyokuwepo na nani aliathirika nacho. Matumizi ya picha yalifanya majadiliano kuwa hai sana. Watu mbalimbali walizitafsiri picha kwa namna

---

<sup>7</sup> Maelezo ya picha zilizotumika na matokeo ya majadiliano yanapatikana katika ripoti ya “Elimu-jumuishi kwa Vitendo”.

<sup>8</sup> Kwa maelezo zaidi tazama ripoti kuu ya “Elimu-jumuishi kwa Vitendo”.

mbalimbali pia, na walikuwa na mawazo tofauti kuhusu nani ameathirika au hajaathirika na kikwazo hicho.

Zoezi la chemsha-bongo la ziada pia lilifanywa wakati huu kuhusu dhana ya vibainishi-mchanganyiko; wazo kwamba kila mtu ana vibainishi vingi na kwamba watu wanaweza kukabiliwa na vikwazo katika ujumuishi kutokana na moja ya vibainishi hivyo. Kwa kuzingatia kuwa washiriki wengi walitoka kwenye projekti/mashirika yanayoshughulikia walemavu, walielezwa kufikiria zaidi vibainishi ambavyo mtu mlemavu anaweza kuwa navyo.

Mazoezi haya yalikuwa muhimu sana kwani yalitoa ujumbe kwamba elimu jumuiishi ni mchakato-tata ambao unahusisha masuala yote ya ulemavu, usadifu wa/kufikika kwa mazingira, na rasilimali.

### **3.5.2. Vielelezo vya mlima**

Zoezi hili linawasaidia wanasemina kufikiria kuhusu:

- Wanataka kupata nini (kufikia lengo lililoko juu kileleni)
- Vikwazo watakavyokabiliana navyo kabla ya kufika kileleni
- Ishara za matumaini walishakutana nazo njiani au mawazo waliyonayo kuhusu kuvikabili vikwazo.

Ni njia nzuri inayoshirikisha zaidi kuzungumzia na kurekodi masuala haya kuliko kushikilia majadiliano na kuandika nukuu. Njia hii hasa hasa inaweza kusaidia wanasemina wanaoona aibu ya kuongea au yule ambae hana uwezo mzuri wa kuandika.


Makundi yaliombwa kuchora mlima kwenye karatasi (za manila). Kileleni kuwe ndio lengo lao, na lengo hilo liwe 'elimu-jumuiishi'. Walielezwa kuongeza njia watakayoweza kutumia kufikia lengo, na waoneshe vikwazo au matatizo ambayo watakumbana navyo au wameshakutana navyo. Waliweza kutumia michoro, alama na/au maneno kuonesha vikwazo. Wanasemina walikumbushwa wasiangalie sana vikwazo vya mazingira na fedha tu. Pia walitakiwa kuonesha ni nani watahathirika kwa kila kikwazo, na ikiwezekana, ni nani anaweza kuwasaidia wao kutafuta habari zaidi kuhusu kila kikwazo.

Katika hatua za mwanzo walijikita zaidi katika kubainisha vikwazo; utatuzi uliingizwa kwenye kielelezo baadaye. Kielelezo kilichokuwepo kilionesha lengo la mradi wa Ukimwi kwa kifipi kama mfano wa dhana (tazama katika mchoro hapa chini)

Wanasemina walipangwa kwenye makundi ya watu wanaotoka nchi moja au yule ambaye anahisi anaweza kufanya nae kazi ya hali halisi ya maisha. Waendeshaji mara ya kwanza walitumia muda kwa kila kikundi kuelezea kazi na kuwahamasisha kufikiria kuhusu vikwazo ambavyo wangekabiliwa navyo katika kufika kileleni. Ilisisitizwa kwamba michoro zaidi ya vikwazo inatuwezesha kuwa wazi – na hivyo kuwa makini zaidi na kufanikiwa – katika kupata ufumbuzi. Muda maalum ulitolewa kwa zoezi hili (siku tatu). Hii iliwawezesha wanasemina kupitia vielelezo vyao kwa kuangalia mawazo waliyopata kutoka kwa wenzao, kutambelea mashule, n.k.<sup>9</sup>

---

<sup>9</sup> Tazama ripoti ya "elimu-jumuiishi kwa Vitendo" kwa maelezo zaidi ya vielelezo vya mlima vilivyochorwa na wanasemina.



Mfano wa kielelezo cha mlima kuhusu mradi wa tahadhari ya UKIMWI

### 3.5.3. Uzoefu binafsi na kuandika

Mara baada ya wanasemina kuchora vikwazo kwenye milima yao, walipewa dakika kumi na tano (15) kutumia uzoefu wao binafsi kuandika bila kujadiliana. Kila mwanasemina alichagua kikwazo kutoka kwenye mchorowao na kuandika mafungu machache kuhusu namna gani wangeweza kutatua kikwazo hicho (au ni jinsi gani walishakitatua).

Mwishoni mwa dakika 15 waendeshaji wa warsha walianza kujadili maandishi ya baadhi washiriki, kutaka kuona kama utatuzi ulikuwa bayana na mahsusi zaidi kiasi cha kujenga misingi ya utatuzi. Kuhakikisha ufumbuzi kama ulikuwa mahsusi, mmoja wa waendeshaji semina alimwomba mwanasemina mmoja asome kwa sauti utatuzi wao. Akiwa anasikiliza maelezo (utatuzi) alishawishika kuchora picha za utatuzi. Kama maelezo hayakutosheleza kuonesha kazi kwa njia ya michoro, mwendeshaji huyo alimwuliza swali muwasilishaji kutafuta maelezo/habari zaidi.

Cha kufurahisha zaidi mmoja wa wanasemina aliandika kipande kidogo cha habari akipendekeza kazi itafsiriwe kama mwaliko na kueleza wafadhili ndani ya chumba ni nini anahitaji kupatiwa. Maelezo katika kipande kile yalimaliziwa kwa kusema “natanguliza shukurani zangu”. Kama ilivyotajwa kwenye kipengere cha 2.7, haya mapendekezo kwamba ‘patner/practitioners’ uwenda pia ikaambatana na namna ya utendaji kwa nia ya kusubiri kukosolewa na mfadhili na labda wakati mwingine kungoja mfadhili apendekeze ufumbuzi. Mazoezi yanayowataka washiriki kutafuta ufumbuzi wao wenyewe kwa kutumia njia mbalimbali zilizo zoeleka zinapaswa kupewa kipeombele ili kuepusha ‘elimu-jumuishi’ kutofuata kanuni/fomyula ngumu.

#### **3.5.4. Maigizo/michezo ya kuigiza**

Kwa kuwa washiriki wametumia muda mrefu kufanya kazi katika michoro ya milima ndani ya nchi zao/washiriki katika kikundi kulikuwa na umuhimu wa kuruhusu kupata nafasi zaidi ya kubadilishana mawazo na kujadili baina ya mataifa na miradi. Zoezi la igizo la mkutano wa waandishi wa habari lilitumika siku ya mwisho. Makundi matatu au manne yalikutana ndani ya chumba kikubwa. Kundi moja liliigiza kama wasaili, huku washiriki wa kundi jingine waliigiza kama waandishi wa habari. Waandishi wa habari walikuwa wanawauliza maswali kuhusu michoro ya mlima ya wasailiwa. Mahsusi, maswali yalilenga kujua ni nini kundi lao limependekeza kutatua tatizo walilochagua, au kupewa taarifa zaidi kuhusu utatuzi uliotajwa kwenye mchoro. Kwanza waendeshaji walionyesha mchezo wa kuigiza ili kuonesha washiriki jinsi inavyotakiwa kuwa.

Zoezi hii lilionekana kuchangamka sana kwani waandishi wa habari waliuliza maswali magumu na yenye mtego. Muundo huu wa maswali uliwashangaza wengi, ingawa sio wote, walitakiwa kuwasilisha kwa kina mawazo yenye upeo wa juu jinsi ya kutatua matatizo mbalimbali. Pia iliwapa nafasi ya kuwasilisha uzoefu wao wa kupambana na elimu-jumuishi. Waandishi wa habari pia waliruhusiwa kutoa maoni yao juu ya utatuzi kwa kuzingatia uzoefu wao au hadithi walizowahi kusikia mahali pengine. Kwa kuwa ufumbuzi mpya ulikuwa umejadiliwa kiasi cha kutosha, wasailiwa waliambiwa kuandika/kuongeza nukuu katika milima yao. Kila kikundi kimoja cha mlima kilikuwa kinachukua dakika 15, kabla ya kupeana majukumu. Zoezi hili lilionesha njia nzuri ya kuchangia matokeo ya majadiliano yaliyofanywa katika vikundi, badala ya kutegemea uwasilishaji uliopangwa kwenye karatasi katika mikutano ya pamoja.

#### **3.5.5. Kutembelea/ziara mashuleni**

Mpango wa kutembelea mashuleni ulifanyika siku ya tatu ya warsha. Mwisho wa siku ya pili kipindi kifupi kiliwasaidia washiriki kuandaa safari hii. Maandalizi haya ni muhimu kuhakikisha kuwa safari za kimasomo ni zaidi ya safari za kitalii. Madhumuni ya ziara mashuleni ni kuwasaidia washiriki kujikumbusha kuhusiana na majadiliano yao juu ya elimu-jumuishi waliyojifunza kwa kuangalia hali halisi ya shule zinazotaribu kuwa jumuishi zaidi. Matembezi haya pia yalitoa nafasi ya kubadilishana mawazo baina ya pande mbili yaani wageni na wenyeji.

Washiriki walielezwa juu ya kaida za ziara mashuleni. Kulikuwa na makundi ya watu 6-7 kwa shule. Walipofika katika shule walizopangiwa kila kundi liligawanyika katika makundi matatu madogo na kufanya mazungumzo katika sehemu tatu zifuatazo:

1. uchunguzi darasani
2. kufanya mazungumzo ya kina na mkuu wa shule, pale inawezekana
3. mazungumzo na walimu/wanafunzi – mmoja mmoja au katika vikundi.

Kazi hizi zilikuwa zikichukua muda wa saa moja kwa jumla, na kufuatiwa na kikao kikubwa cha walimu na wawakilishi wa jamii au wazazi.

Kila kikundi kilikuwa na muhamasishaji mmoja au wawili. Hawa hawakupaswa kuwa wenyekiti au waendeshaji. Kazi yao kubwa ilikuwa ni kusaidia jinsi ya kuanza mazungumzo kama watu hawataweza kuongea, au kuwakumbusha washiriki mazoezi matatu kama wakisahau la kufanya. Wahamasishaji walichaguliwa na mwendeshaji kuhakikisha kuwa kila kikundi kinakuwa na muhamasishaji kutoka kaskazini au kusini. Makundi pia yaligawanywa na waendeshaji kuhakikisha uwakilishi wa kaskazini na kusini uko sawa katika kila kikundi; na kuwapa kila kikundi mtu ambaye anaongea Kiswahili na ambaye angeweza kuwa kama mkalimani kama inawezekana.

Shule zilizotembelewa zilikuwa zimekwishataarifiwa kupitia Chama cha watu wenye ulemavu Zanzibar na wafanyakazi wa wizara kuwa wageni walitarajia kuziona shule 'kivitendo'. Waliombwa kutofanya maandalizi rasmi ya mapokezi, vinywaji/burudani, na maonyesho, kwa sababu hivi vingeharibu malengo halisi ya ziara hizo.

#### Uchunguzi wa darasa

Uchunguzi wa darasani ni kuhusiana na kuangalia na kusikiliza kwa makini. Ni wazo zuri la kuandaa maswali katika karatasi mapema ambayo unataka kuyachunguza kama (tabia, mahusiano, rasilimali, njia za ufundishaji, n.k.) na ilikuwa vizuri pia kuandika wakati wa uchunguzi, inaweza ikafanyika kimya bila ya kumwingilia mwalimu au mwanafunzi. Washiriki walioneshwa mbinu moja inayoweza kuwa ya kuchukua nukuu ambayo inahusisha kugawanya ukurasa katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

<b>Mambo bayana uliyoyaona</b>	<b>Mawazo na uchambuzi kuhusu uchunguzi</b>
Wavulana tu ndio wanaongea darasani	Kwa nini mwalimu hawaulizi wasichana? Anaonekana anawatenga wasichana

Mbinu hii itakusaidia utakapoangalia nukuu zako hapo baadae – hasa unapotaka kulinganisha namna watu wengine walivyochambua utafiti huo.

Wakati wa kipindi cha maandalizi ya kufanya ziara mashuleni, washiriki walichangia orodha ya mambo ambayo walitaka kuyaangalia wakati wa uchunguzi darasani (tazama hapa chini). Viongozi walishauriwa kufikiria vitu vingine vya ziada ambavyo wangevichunguza wakati wa ziara hizo.

- idadi ya wanafunzi
- usadifu wa mazingira
- tabia za walimu kwa wanafunzi
- jinsia, Ulemavu na mambo mengine kwa watoto – na ushiriki wao
- mpangilio wa ukaaji wa darasani

- njia za ufundishaji
- samani za ndani
- ugawaji wa vifaa vya kujifunza na umuhimu wake
- tabia ya wanafunzi
- uwiano wa wanafunzi na walimu
- mazoezi ya wanafunzi-jinsi gani wanashughulishwa/shirikishwa.

Walikumbushwa kuwa hawataweza kuangalia kila kitu kwa muda mfupi, isipokuwa watengeneze orodha ya mambo ya kuchunguza.

Kuongea na walimu, wanafunzi na mkuu wa shule.

Washiriki walikumbushwa kuwa ni muhimu kujiandaa hata kwa mahojiano yasiyo rasmi. Ingawa hakutakuwa na mpangilio wa mahojiano mashuleni, walishauriwa kufikiria baadhi ya maswali kabla – vitu ambavyo walitakiwa kujua kuhusu shule na ujumuishi Zanzibar. Washiriki pia walikumbushwa kubadilishana uzoefu wao na mawazo na wenyeji mashuleni, na kwa hiyo watafakari usiku huo masimulizi na uzoefu wao watakaowaambia wenyeji wao. Baada ya safari hiyo wataulizwa angalau jambo moja walilofunza na uzoefu mmoja au wazowalilobadilishana wakati wa ziara.

Taarifa-rejea/tathmini (*feedback*)

Kipindi kirefu cha tathmini kilifanyika mchana baada ya kurejea toka ziarani.<sup>10</sup>

Kwanza, kila mshiriki alipewa karatasi ya ngumu ya data na kutakiwa kuorodhesha kitu kimoja walichojifunza wakati wa ziara na kitu kimoja walichobadilishana mawazo na wenyeji. Katika makundi yao ya shuleni, washiriki kasha walijumuika kujadili na kufanya tathimini ya kina. Kila kikundi kilipewa karatasi yenye maswali yafuatayo:

1. Je shule ilionekana ukilinganisha na shule yako/zako?
2. Shule hiyo ilitofautianaje na shule yako/zako?
3. Je ni vikwazo gani vya ujumuishi ulivyoviona au kusikia watu wanaviongelea kuhusu shule hii?
4. Je ni utatuzi gani wa matatizo uliuona au kusikia watu wakiongelea kuhusu shule hii?
5. Ni kitu gani kimekufurahisha sana au umejihusisha nacho zaidi ambacho utaenda kusimulia wafanyakazi wenzako nyumbani?

Walihamasishwa kujadiliana mambo waliyoyachunguza na walichoandika na uhalisia katika nchi wanazotoka ili kujibu maswali haya. Kulikuwa na mjadala wakusisimua na makundi mengi yalijaza kirahisi karibu karatasi za majibu 5 au 6. Ilidhihirika wazi kuwa hata katika nchi tofauti washiriki kulikuwa na baadhi ya mambo yaliyo sawa na yale yaliyoonekana katika shule za Zanzibar kutokana na uzoefu wao. Kulikuwa na ukosefu wa muda kiasi kwamba baadhi ya vikundi havikutoa taarifa-rejea (tathmini) ya uchunguzi wao kwenye mkutano wa pamoja. Bahati nasibu ilitumika ambapo kila kikundi kilichagua karatasi yenye namba na kuwasilisha jibu lao kutokana na swali lililo ulizwa. Ilieleweka kutoka katika majadiliano na uwasilishaji kuwa ziara yao ya mashuleni imewasaidia sana kugundua na kujadiliana kwa upana zaidi kuhusiana na 'elimu-jumuishi' ambapo ilionekana ni zaidi ya masuala ya ulemavu, rasilmali, na kuwepo kwa mazingira sadifu.

<sup>10</sup> Tathmini yote iliyotolewa na wanasemina inapatikana kwenye 'document' inayojitegemea.



## 4. Mazoezi ya chemsha-bongo

Mazoezi yafuatayo yalifanyika wakati wa kipindi chote cha warsha. Baadhi yalikuwa ni mazoezi ya furaha na kuvunja ukimya na mengine yaliambatana na vielelezo vya ujumbe kulingana na dhamira ya elimu-jumuishi.

### 4.1. Michezo ya furaha ya kuvunja ukimya

#### ***Maboya ya kuokolea***

Zoezi hili liliwafanya watu watembee na pia liliwasaidia waendeshaji wa warsha kuwachanganya watu katika makundi tofauti tofauti. Wanasemina walisimama katika eneo la wazi na kuanza kutembea kwenye duara ( kutembea kwa mzunguko) na waliambiwa ya kwamba wamo katika meli inayozama. Maboya ya kuwaokoa yanaletwa, lakini yana uwezo maalumu wa kuokolea (kubeba). Pale mwendeshaji wa warsha anaposema kwa sauti “maboya haya hapa, uwezo wake ni watu 3”, washiriki mara moja wanatakiwa wajikusanyea katika kundi la watu watatu. Zoezi hili linaweza kufanyika mara nyingi kwa idadi tofauti ya vikundi vinavyotajwa mpaka pale watapofikia idadi kamili ya kundi linalohitajika kwa zoezi inayofuata.

#### ***Tahijia za mwili***

Zoezi hili ni la kasi na jepesi la kumwamsha aliyelala/kuzubaa, hasa lilifanyika wakati wa kuelekea mwishoni mwa kipindi. Washiriki waliombwa kutaja tahijia za neno fupi, lililotolewa na mwendeshaji, bila kuongea au kutumia mikono na viganja. Walitumia vichwa kuzungusha ili kutengeneza maumbile ya herufi.

#### ***Kujiburudisha wenyewe***

Wanasemina waliombwa wajifanyea kana kwamba wamegawiwa chupa za soda. Lazima wakamate chupa, wafungue hizo chupa na opena, na kunywa soda (waoneshe msisitizo wa sauti kwa kila kitendo).

#### ***Nini kimebadilika?***

Washiriki hukaa katika jozi. Lazima watumie sekunde chache kutazamana; na kisha hupeana migongo, na lazima waoneshe kitendo kimojawapo tofauti baina yao (mf. kuondoa mawani). Pale watakapo geuka na kutazamana uso kwa uso kila mmoja tena hulazimika kugundua/kubaini ni nini kimebadilika kwa mwezake.

#### ***Kuwa mkweli/mwema/mzuri/safi***

Washiriki hukaa katika jozi tena. Hulazimika kusema kwa haraka kitu cha kumfariji mwenzake.

## 4.2. Michezo kuvunja ukimya inayohusisha elimu-jumuishi

### ***Hakuna mukaka, hakuna mbolea.***

Kwa lugha ya kabila la wa-Bemba la nchini Zambia ‘mukaka’ maana yake maziwa. Zoezi hili linawataka wanasemina kutazama picha ya mtoto – (wa kike) anawenda shule, na yuko peke yake. Tunamfikiriaje huyu binti? Ni kitu gani muhimu kwake? Namna anavyowasiliana na watoto wengine ndio kitu muhimu kwake. Michezo ni kitu muhimu sana kwake pia. Inampa motisha na nguvu (hii ni sawa na pasipo mukaka/maziwa, hakuna mbolea!). Muwendeshaji wa warsha aliwafundisha wanasemina kuimba wimbo “Hakuna mukaka, hakuna maziwa!” Walitembea kwa duara na kuimba wimbo kwa kumfuata mwendesha warsha namna alivyokua akicheza kwa kuongeza kasi na nguvu zaidi.

### ***Vituo vya safari***

Zoezi hili ni la kupasha mwili nguvu na kuvunja ukimya, lakini pia linawafanya washiriki kuweza kuzungumza na watu ambao hapo awali hawakuzungumza nao katika muda wa warsha, na kuwasaidia kukumbuka kupitia mafunzo na mawazo yao kwa undani. Washiriki wanasimama kwenye mizunguko miwili ya duara, moja ndani ya nyingine. Watu katika kundi la ndani wanasimama kama walivyo (wao ndio vituo). Kundi la nje linaanza kuzunguka (wao ni garimoshi). Baada ya muda mwezeshaji anasema ‘SIMAMA!’ na wanasemina wanaozunguka wanalazimika kusimama katika kituo karibu ya mtu aliye naye. Wanasemina ambao ni gari moshi ni lazima waseme kwa wanasemina ambao ni kituo kuhusu kituo kilichochaguliwa na mwezeshaji wa semina. Kwenye hii warsha tumechagua wanasemina kuzungumzia kuhusu ‘nimejifunza nini mpaka sasa katika warsha’. Bada ya dakika moja wanasemina ambao ni gari moshi tena wanaanza kuzunguka mpaka kwenye kituo kinachofuata na wanasimama pale wanapotangaziwa tena. Miduara hiyo inaweza kubadilishana ili kwamba kila mshiriki aweze kupata nafasi ya kuwa gari moshi na kituo.

### ***Duara la ubaguzi***

Zoezi hili linasaidia kuonesha namna ubaguzi ulivyo duara. Katika jamii kuna ukiritimba, hakuna haki, na kuna ubaguzi. Watu wanaozaliwa katika mfumo huu hujifunza kuhusu tabia zote hizi na hivyo duara linaendelea kuzunguka. Tunatakiwa kulivunja duara –tusimamishe mzunguko wa duara, tuzuie watu kuamini ubaguzi na ukilitimba – kama tunahitaji kutengeneza jamii ambayo kila mmoja atajumuishwa.

Washiriki wanasimama kwenye duara na kuendelea kuzunguka. Wachache huchaguliwa kusimama nje ya duara; huambiwa ni lazima wazuie mzunguko wa duara. Wanaweza kutumia ushawishi, ucheshi, busara, ujanja wa kuomba, utu, n.k (lakini si ugomvi wala fujo) kufanya watu waache kuzunguka na hivyo duara litakuwa limevurugwa. Zoezi hili linasaidia kuonesha njia mbalimbali ambazo tunaweza kutumia ili kukomesha duara la ubaguzi na uonevu kwenye jamii. Tunaweza kutumia ushauri, ushawishi, elimu, ngoma, sanaa za maonesho n.k. kusaidia kubadilisha mtazamo wa watu na tabia na hivyo duara linadhoofika na hatimae kuvunjika.



# Viambatisho

## Kiambatisho cha 1: Matumaini na mashaka ya washiriki kuhusu warsha

Kabla ya warsha washiriki walijaza maswali ya dodoso ambayo yalijumuisha nini walichotaka kujifunza zaidi katika warsha na nini kilichowashughulisha mpaka kushiriki warsha.

### Matumaini

Matumaini ya kujifunza yanaweza kugawanyika kwenye makundi na kufupishwa kama ifuatavyo:

#### ***Kubadilishana uzoefu/mawazo (watu 16)***

- kujifunza uzoefu wa wengine
- kusikiliza na kulinganisha matatizo.
- kubadilishana mawazo na vifaa
- kujadiliana vikwazo na ujumuishi kutoka kwa wengine
- kufanya mawasilino kwa ajili ya baadaye kuhusu mawazo, vitabu, vifaa, n.k

#### ***Kutaka kupata habari za msingi (watu 4)***

- Nini maana ya elimu-jumuishi?
- Kwa nini elimu-jumuishi?
- Nini matokeo ya elimu-jumuishi na mara kwa mara ni yapi majibu?

#### ***Kuanzisha kwa elimu-jumuishi (watu 6)***

- Namna ya kupanga, kutekeleza, na kutathmini miradi ya elimu-jumuishi.
- Namna ya kuanza tangu ngazi ya wilaya hadi ya taifa?

#### ***Njia za vitendo za kufundishia/kuwasaidia watoto wenye ulemavu (watu 6)***

##### ***Mada zingine zilizojitokeza:***

- majukumu ya wazazi, mashirika yasiokuwa ya kiserikari, serikari
- jinsi ya kupata ushirikiano kutoka serikalini, n.k.
- jinsi ya kuhakikisha elimu-jumuishi inabaki ndani ya sera ya
- elimu, hata baada ya mafungu ya fedha kusimama.
- fedha / rasilimali
- misaada.

##### ***Masuala maalum ya elimu jumuishi:***

- ulemavu wa moja kwa moja
- ulemavu wa kutosikia
- VVU/UKIMWI
- matatizo ya akili
- matumizi ya walimu mahiri na wazoefu

- mipango ya wanaomaliza shule na elimu ya watu wazima/kujifunza kusikokoma.
- jinsi mbinu au njia ya mtoto kwa motto inavyofanya kazi darasani.
- jinsi elimu-jumuishi inavyoboresha elimu kwa hata wasio walemavu.
- matumizi ya tathimini ya mtu mmoja mmoja na mipamgo yake ya kujifunza-katika kituo/shule za nchi maskini.

## Woga/mashaka

Woga au mashaka yanaweza kupagwa na kufupisha kama ifuatavyo:

- Muda** Tunaweza kufundisha mada zote kwa wakati wake. Je, ziara itatosha ndani ya muda uliopagwa?
- Tajiriba/uzoefu** Woga wa kufikiri kuwa sina mambo ya kuchangia kwa washiriki wenzangu? Ninatoka nchi ambayo elimu-jumuishi ni kidogo sana au hakuna kabisa. Je nina ujuzi mdogo kuliko wenzangu?
- Majadiliano** Je uzoefu/mambo yetu yatakuwa segemnege sana hata tusiweze kuyasawazisha? Je wenzetu wataafiki tuliyofanya? Je kutakuwepo na kusigana wakati wa kuchangiana uzoefu Je majadiliano yatakuwa tofauti sana au ya juu zaidi? Je uzoefu wa kazi au nchi zetu utatofautiana sana? Je kila mmoja atajihusisha na kujadili matatizo badala ya kutafuta ufumbuzi?
- Maoni** Je itawezekana kuepuka kutoa maoni yasiyofaa?
- Kiini/yaliyomo** Wasiwasi wa kuwa warsha inaweza isijihusishe kikamilifu na ulemavu au matatizo ya kiakila badala yake ikijikita na ulemavu matatizo ya kimaumbile
- Mengineyo** Uhaba wa karatasi zilizotolewa na kanda za kusikiliza. Watu wenye nafasi au vyeo vyao hawataweza kuchagizwa ili kueleza mipango yao.

Wengi wa washiriki hawakuwa na woga wala wasiwasi.

## Kiambatisho cha 2: Mtandao bayana (swap-shop networking)

Majibu yafuatayo yaliandikwa na washiriki kwenye vikaratasi (post-its) wakati wa zoezi hili. pale ilipowezekana, tumeingiza na majina ya waliotoa maoni husika. Tunawashauri wanasemina kuendelea na mazoezi hili – kama utamwona mtu kwenye orodha hii anaweza kujibu swali lako au ana swali ambalo unaweza kujibu – kisha jitahidi kuwasilana naye au nao.<sup>11</sup>

### Kuhusiana na elimu-jumuishi, ninafahamu/ninaweza kusaidia.....

- Jinsi ya kuratibu shughuli za elimu wilayani (Ahmed).
- Kuzungumzia kuhusu uzoefu wangu kwa kutumia kanda za video kubadilishana na wenzangu kuhusu vijarida (Bronchure) vinvyohusu ujumuishi katika kambi za majira ya joto/kiangazi (Akram).
- Mipango ya utekelezaji, uhamasishaji wa wazazi (Beda).
- Uzoefu wa kuwahi kuwa mwanafunzi katika shule jumuishi na kufanya kazi na elimu –jumuishi kwa mwaka ( Bergdis).
- Maoni ya wazazi. Ujumuishi ni nini? Ni jinsi gani mashirika yasiyo ya serikali NGOs yahnaweza kusaidia elimu-jumuishi-mfumo wa wazazi (Bikko Ragna Langlo).
- Kutoa msaada wa hali na mali kutekeleza elimu-jumuishi (Doya).
- Uzoefu wangu wa miaka 18 kama mwalimu. (Edwina)
- Jinsi ya kuendeleza kozi ya msingi kabla ya kutekeleza elimu –jumuishi. (Evena).
- Baada ya mawazo kuhusu kuwamotisha walimu. (Geir).
- Vikwazo vya elimu-jumuishi. Kufikika/kupatikana kwa majengo katika shule jumuishi. (hamadi).
- Kunahitajika nini ili kuanzisha elimu-jumuishi, na jinsi gani ya kutangaza na kushawishi umma.
- Jinsi ya kuwatayalisha /kuwahabarisha wanafunzi, wazazi na jamii. (Henry).
- Jinsi ya kuanza na namna ya kuwapata maafisa jamii ili wafanye kazi kwa kushirikiana na maafisa wa elimu. (Johan).
- Kubadilishana mawazo kuhusu kuwahasisha maafisa elimu. Kuwapa mafunzo walimu wa kawaida kuhusu elimu-jumuishi. Kubadilishana mawazo na uzoefu kuhusu namna ya kuanzisha elimu-jumuishi katika shule /darasa la kawaida. (Kalumuna)
- Uzoefu kuhusu mipango endelevu ya kutekeleza elimu-jumuishi. (Lillian)

---

<sup>11</sup> Maelezo kuhusu anwani za washiriki wa warsha hii yanapatikana katika ripoti kuu ya warsha: “Elimu-jumuishi kwa Vitendo”.

- Namna ya kuhusianisha watu wenye ulemavu nchini Norway. Mahali shirika la “Atlas Alliance” linapofanya kazi ya elimu-jumuishi; na sio zaidi.(Line)
- Mimi ni mwalimu (Mkufunzi) wa elimu maalum. Nabadilishana uzoefu kwa kutoa uchambuzi/ufafanuzi/mbinu ya kuwachuja. (Matemoho).
- Maarifa ya namna ya kufanya kazi na jamii ya watu walemavu (Mathabo).
- Ujuzi wa kufundisha walimu kuanza elimu-jumuishi, utengenezaji wa vifaa vya kujifunza /kufundishia, kuboresha mazingira ya kujifunza /kufundisha watoto wote (Menya).
- Uzoefu wa tabia katika jamii ya walemavu na elimu-jumuishi (Mpaji).
- Umuhimu wa elimu-jumuishi kwa kila mtu, jamii na maendeleo ya taifa. Umuhimu wa kuwashirikisha wadau wote katika mipango ya elimu-jumuishi. (Mussa).
- Uzoefu wa kuanzisha elimu-jumuishi katika nchi yetu.(Mwanaidi).
- Maana /umuhimu wa elimu-jumuishi, hasara za utengano(Noel)
- Kusaidia jinsi ya kushughulikia masuala ya CRB (Nthma)
- Tunahitaji sasa kuanzisha elimu-jumuishi (obeid)
- Namna gani tunaweza kutengeneza vifaa vya nyumbani (rahisi) kwa watoto wenye matatizo ya ulemavu (Owenodumo)
- Namna mradi wa elimu-jumuishi wa Mpika unavyofanya kazi Zambia. (Patrick)
- Kubadilishana habari kuhusu rasilmali zilizopo na zipi zinafaa katikasera na utekelezaji wake. (Ragnhild)
- Kubadilishana uzoefu kutoka kwa watu wengine kuhusu elimu-jumuishi katika eneo langu la kazi.(Samson)
- Uzoefu pamoja na kubadilisha shule maalum kuwa vituo vya rasilmali kwa shule-jumuishi; uzoefu pamoja na kuelimisha walimu wa elimu-jumuishi.(Siri)
- Uzoefu wa siku nyingi kutoka CRB nchini Uganda, serikali/jamii.(Svein)
- Namna ya ketekeleza elimu-jumuishi.(H.Tbuye)
- UJuzi wa kusimamia miradi inayoshughulikia wanafunzi wenye matatizo ya kusikia.(Tommy)
- Uzoefu kutoka elimu ya lugha mbili. (Trond)
- Kuanzisha mara moja elimu-jumuishi katika serikali za mitaa.(Wadenya charles)
- Ninaweza kusaidia baadhi ya vifaa vya kujifunza, ili kuanzisha elimu-jumuishi Zanzibar. (Wadi)

## **Kuhusiana na elimu-jumuishi nataka kufahamu.....**

- Kusikia kuhusu uzoefu wa walimu. Namna gani wizara inatekeleza elimu-jumuishi?
- Ni jinsi gani Wizara ya Elimu imeshawishika kuhusiana na hili?
- Ni jinsi gani watachanganywa watoto viziwi na vipofu katika madarasa ya kawaida.
- Ni jinsi gani walimu watapeleka motisha ya kuwatunza watoto wenye mahitaji maalum. Kuanzisha/kuendeleza staid za lugha ya ishara .(Ahmed)
- Kufahamu uhusiano kati ya elimu-jumuishi na elimu maalumu; mwalimu atafanya nini ndani ya darasa kwa wanafunzi wanaoelewa taratibu na wanafunzi walemavu.(Akram)
- Kupangilia mipango na kuwezesha mikakati ya kitaifa.(Beda)
- Ni jinsi gani unavyoweza kushughulikia elimu-jumuishi katika shule yenye watoto wengi.(Bikko)
- Nini maana ya elimu-jumuishi; kwa nini tuitekeleze; na jinsi gani tunaweza kuitekeleza?(Doya)
- Mawazo zaidi kuhusu jinsi gani watu wanaifaya katika nchi nyingine.(Edwina)
- Ni jinsi gani unaweza kuwasaidia viziwi na walio na matatizo ya kujifunza katika mazingira ya darasani.(Ellena)
- Ni jinsi gani utawabadilisha tabia wanaotengeneza sera.(Evena)
- Ni jinsi gani utawapa motisha walimu; ni jinsi gani utaweka elimu-jumuishi kwa vitendo.(Geir)
- Njia zilizotumika katika elimu-jumuishi; ni jinsi gani tutatengeneza sera?(Hamadi)
- Ni jinsi gani ya kuandika sera juu ya elimu-jumuishi? Ni jinsi gani tutasaidia watoto wenye ulemavu kwa kiwango cha sekondari na elimu ya juu.(Henry)
- Ni jinsi gani tutaanzisha mtaala ambao ni jumuishi, lakini hauwapunguzii watoto wala kuondoa matatizo ya kujifunza kwa haraka wanavyoweza. Mimi ni mgeni katika sekta ya elimu-jumuishi. Nina hamu ya kujifunza kutoka kwa watu wazoefu katika fani hii.(Jennifer)
- Njia mbalimbali za ufundishaji ambazo ni shirikishi zaidi; ni jinsi gani watoto wasiokuwa walemavu watakuwa wamefikia mwisho zaidi wa kujifunza kwa mabadiliko zaidi ya njia mbalimbali na za kujifunza katika ujumuishi .(Johan)
- Ni jinsi gani watu wengine wanavyopanga mipango na program ya elimu jumuishi.(Kulumuna)
- Ni jinsi gani watu wanahusisha elimu kwa wote na elimu-jumuishi; ni jinsi gani utawashirikisha watu mabimbali wenye ulemavu katika elimu na maisha ya kila siku.(Lillian)

- Kwa ujumla wa elimu-jumuishi mimi ndio 'naanza'. Ni jinsi gani ujumuishi kwa kweli unafanya kazi kwa vitendo – na je watu katika nchi zinazoendelea wanauamini?(Lina)
- Nini maarifa ya msingi yanayoweza kupendekezwa bungeni (Kuhusiana na ulemavu)
- Ni jinsi gani wanafunzi wenye matatizo ya tabia na mwenendo wanaweza kupata msaada mzuri katika mazingira-jumuishi.(Matemoho)
- Ni jinsi gani utawashirikisha wanafunzi walemavu zaidi katika madarasa ya kawaida; kwa mf. Wenye mtindio wa akili, ulemavu wa viungo (Mathabo)
- Ni jinsi gani ya kufanya mtandao na wengine wanaotoa elimu-jumuishi. Njia bora za kutumia utekelezaji. Kupanga mipango thabiti ya warsha ya elimu-jumuishi kwa walimu wote.(Menya)
- Ni jinsi gani unaweza kuwatunza /kuwahudumia watoto wenye ulemavu tofauti ndani ya darasa-jumuishi. Ni jinsi gani utawahudumia watoto wenye matatizo ya kiakili ndani ya mazingira-jumuishi ya kijifunza. (Mpaji)
- Mikakati bora ya kuwashirikisha wadau mbalimbali katika elimu-jumuishi.Njia bora za kuwashirikisha wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali katika masomo. (Mussa)
- Hamasisha jamii ili ikukubali na kuiendeleza elimu-jumuishi. (Mwanaidi)
- Ni jinsi gani sera na sheria vinaweza kubadilika na kuwezesha ujumuishi.(Noell)
- Ni jinsi gani unaweza kuwashughulikia wasiosikia vizuri katika darasa madarasa ya kawaida. (Nthma)
- Jinsi elimu-jumuishi inavyofanya kazi katika nchi mbalimbali.(Obeid)
- Njia za kufundishia watoto katika ya elimu-jumuishi.(Owerodumo)
- Ni jinsi gani nchi nyingine zinafanya kuanzisha elimu-jumuishi.(Patrick)
- Walimu wa shule maalum hawana nia ya kuanzisha program ya elimu-jumuishi, sababu wanaogopa kupoteza kazi zao; kwa hiyo napenda kufahamu ni namna gani mmewatia moyo kuanzisha programmu hii.(Promilla)
- Kuhusiana na vikwazo vya elimu-jumuishi, ni vikwazo gani vilivyosugu sana katika bara zima au nchi? Jinsi gani tunaweza kuvitatua au kuviondoa.(Ragnhild)
- Uongozi wa darasa. Habari zaidi kuhusu elimu-jumuishi.(Shauri)
- Mifano ya mafanikio katika mageuzi ya elimu ya walimu maalum katika elimu-jumuishi. Mf. ni utaratibu wa vituo vya huduma kwa ajili ya elimu-jumuishi.(Siri)
- Ni jinsi gani elimu-jumuishi inapangiliwa kwa vitendo katika mashule na jamii (Svein)
- Ni jinsi gani tutawafanya wazazi waandikishe watoto wao walemavu shule. (H.Tilya)
- Napenda kufahamu ni jinsi gani mwalimu anaweza kufundisha darasa la watoto wenye ulemavu tofauti kwa urahisi.(Tommy)

- Ni jinsi gani tunaweza kuboresha mtaala wa elimu-ualimu. (Trond)
- Hata kama elimu-jumuishi itaweza kuongeza nafasi za ajira kwa watu walemavu .wadenya Charles)
- Ni jinsi gni tunaweza kufundisha darasa kubwa lenye zaidi ya wanafunzi 80 na walemavu 5 kwa wakati mmoja na kwa ufanisi.(Wadi)

## Kiambatisho cha 3: Mapendekezo ya marejeo ya kusoma

Marejeo yafuatayo yanatoa mawazo ya kuendesha matukio-ushiriki na/au warsha ambazo zinahusisha masuala ya ujumuishi, pasi-ubaguzi, na ushirikishaji wa watu mbalimbali.

“Access for All: Helping to make participatory processes accessible to everyone” [Uwezekano kwa wote kutoa msaada kwa washiriki kuweza kuwa na uweza wa kujisaidia] (Save the Children UK, 2000)

Kitabu hiki kinatoa ushauri wa kufanya mikutano inayowezekeka kwa upana zaidi kwa wanasemina. Kinaonyesha uzoefu wa moja kwa moja kutoka katika ushiriki wa semina ya dunia iliyoandaliwa nchini Swaziland. Maelekezo yanapatikana kwenye CD-ROM EENET, au kwenye mtandao wa kompyuta wa [www.eenet.org.uk/key\\_issues/communication/communication.shtml](http://www.eenet.org.uk/key_issues/communication/communication.shtml). Inapatikana kwa Kiingereza kwa maandishi makubwa, kiarab, kifaransa, Kireno, na kiispania.

“Inclusive education study tours: Lessons learned from an EENET-facilitated study tour, Mpika, Zambia, May 2005” [Safari za mafunzo ya elimu-jumuishi: mafunzo waliyojifunza kutoka EENET-yaliwezesha safari za mafunzo] (EENET, 2005)

Maelezo ya ripoti kwa ufupi yanaonesha uzoefu wa kuandaa safari za mafunzo kwa maafisa elimu kutembelea Zambia kutoka Ethiopia. Yametolewa mapendekezo muhimu na wengine wanaotumaini kufanya safari za mafunzo-shirikishi na kamilifu, kwa wote, wenyeji na wageni. Ripoti hii inapatikana katika nakala halisi kutoka EENET, au mtandao wa kompyuta: [www.eenet.org.uk/key\\_issues/action/action.shtml](http://www.eenet.org.uk/key_issues/action/action.shtml)

“Learning from Difference: An action research guide for capturing the experience of developing inclusive education” [Kujifunza kutokana na tofauti Maelekezo ya utafiti-kwa-vitendo umeonyesha, uzoefu wa maendeleo ya elimu jumuishi] (EENET, 2005)

Mwongozo huu unawawezesha wataalam na wanajamii kuaksi na kurekodi uzoefu/matendo yao, na kisha kujenga mawazo mapya na kufanya matendo/mazoezi mapya ili kuifanya elimu iwe jumuishi zaidi. Unatumia mazoezi-shirikishi sawa na yale yaliyotumiwa wakati wa warsha ya ‘Elimu-jumuishi kwa Vitendo’. Mwongozo huu unapatikana kwenye CD-ROM au printi (CD-ROM ina vifaa vingine vya zaidi kama vile usuli katika kusoma, klipsi za video na za kusikiliza bila video, n.k.).

“Making a Difference: Training materials to promote diversity and tackle discrimination” [Kufanya mabadiliko: Vifaa vya kufundishia ili kuchochea utandawazi na kupambana na ubaguzi] (Save the Children UK, 2005)

Vijarida vya mafundisho haya muhimu huchangia mawazo mengi kwa washiriki katika shughuli za warsha, kazi kama hizi huenda zikatumika kama matumizi ya kozi za moja kwa moja bila ubaguzi na uwazi, au kazi za watu wachache zinaweza kuchaguliwa na kutumika kwa kipindi chote cha warsha na semina.



Maelekezo yanapatikana katika CD-ROM kutoka EENET, au kwenye tovuti ya [www.eenet.org.uk/bibliog/scuk/scuk\\_home.shtml](http://www.eenet.org.uk/bibliog/scuk/scuk_home.shtml).

*Ili kupata nyaraka hizi kutoka shirika la 'EENET', tafadhali wasiliana na:*

EENET - The Enabling Education Network

c/o Educational Support and Inclusion

School of Education

University of Manchester

Oxford Road

Manchester M13 9PL

UK

Barua pepe: [info@eenet.org.uk](mailto:info@eenet.org.uk)



the  
**atlas**  
alliance

global support to  
disabled people

**The Atlas Alliance**

Schweigaardsgt 12  
PO Box 9218 Grønland  
0134 Oslo, Norway  
Tel: +47 22 17 46 47  
Fax: +47 23 16 35 95  
Email: [atlas@atlas-alliansen.no](mailto:atlas@atlas-alliansen.no)  
[www.atlas-alliansen.no](http://www.atlas-alliansen.no)



OPERASJON  
DAGSVERK